



Picha 5: Ugonjwa wa Batobato.

## 7.2 Wadudu

**Vidung'ata, Vidugamba** na **Panzi** hushambulia majani na shina la muhogo, **utitili wa kijani** hushambulia majani machanga. **Mchwa** hushambulia shina. Kudhibiti wadudu waharibifu inashauriwa kupuliza sumu za kua wadudu



Picha 6: Nzi weupe (husambaza magonjwa ya batobato na michirizi kahawia

## 8.0 Uvunaji wa Muhogo

- Muhogo huanza kukomaa kuanzia miezi 9 hadi miezi 12 toka kupandwa.
- Muhogo huvunwa kwa kutumia jembe la mkono au mashine maalumu.
- Uvunaji hufanyika kwa kuchimba, kung'oa shina lote au kutoa baadhi ya mihogo na kuacha shina liendelee pale shambani.



Picha 7: Mkulima akifurahia mavuno.

## 9.0 Usindikaji na masoko

Usindikaji huongeza thamani na fursa za masoko. Inashauriwa kusindika muhogo ili kupata unga bora na wanga. Unga wa muhogo hutumika kutayarisha bidhaa mbalimbali hususani vitafunwa kama mbadala wa unga wa ngano.



Picha 8: usindikaji wa Muhogo.



## KILIMO BORA CHA MUHOGO



### Kimetayarishwa na.

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania  
TARI - Naliendele  
S. L. P. 509,  
MTWARA.

Email : [cdnaliendele@tari.go.tz](mailto:cdnaliendele@tari.go.tz)

April 2019

# KILIMO BORA CHA MUHOGO

## 1.0 Utangulizi.

Muhogo ni miongoni mwa mazao makuu ya chakula nchini Tanzania. Inakadiriwa kuwa tani milioni tano (5) za muhogo mbichi zinazalishwa hapa nchini kwa mwaka. Kanda zinazoongoza kwa uzalishaji ni Kanda ya ziwa (37%), Kanda ya kusini (28%) na Kanda ya mashariki (12%). Karibu 75% ya muhogo unaozalishwa hutumika kwa chakula. Muhogo huvumilia ukame na pia hufanya vizuri hata katika ardhi yenye rutuba hafifu ukilinganisha na mazao mengine.

## 2.0 Kutayarisha shamba

- Muhogo hustawi zaidi kwenye udongo tifutifu wenye rutuba ya kutosha.
- Fyeka na kung'oa visiki kisha tifuia udongo vizuri kabla ya msimu.
- Andaa matuta vizuri ili kuongeza tija na kurahisisha uvunaji na palizi.
- Unaweza kuandaa sesa iliyotifuliwa vizuri

## 3.0 Kuchagua mbegu bora za muhogo

Inashauriwa kitaalamu kutumia mbegu bora zilizoainishwa kitaifa na Taasisi ya utafiti wa kilimo Tanzania kwa ajili ya kutumika katika kanda mbalimbali za uzalishaji:

- Ukanda wa Pwani aina zinazofaa ni **Mkumba, Pwani, Kiroba, Mkuranga1, Chereko, Kizimbani na Kipusa.**
- Mbegu zinazofaa Kanda ya kati ni **Hombolo, Dodoma, Makutupora na Mumba.**
- Kanda ya Ziwa na ile ya Magharibi ni **Mkombozi, Kyaka, Meremeta, Belinde, Nyakafulo, Suma, Kasala na Rangi mbili.**
- Zanzibar na Pemba ni **Kizimbani, Mahonda, Machui na Kama.**



Picha 1: Mbegu bora ya muhogo aina ya Kiroba

## 4.0 Kupanda muhogo

- Upandaji unaostahili ni kufukia pingili tatu hadi nne za muhogo ardhini kwa kuilaza mshazari kidogo.
- Shindilia udongo kando ya shina ili ijishike vizuri ardhini.
- Umbali kutoka mstari mmoja hadi wa pili ni mita 1 na pia mita 1 toka mmea hadi mmea.
- Pia umbali kutoka tuta hadi tuta ni mita moja na mmea hadi mmea ni mita moja.
- Kwa uzalishaji wa mbegu, tumia nafasi ya mita 1 mstari hadi mstari au tuta hadi tuta na nusu mita (sentimita 50) toka mmea hadi mmea.




Picha 2: Upandaji wa muhogo

## 5.0 Matumizi ya mbolea:

Inashauriwa kuchagua shamba lenye rutuba ya kutosha ili kupata mavuno mengi. Utafiti wa matumizi ya mbolea unaendelea kufanyika chini ya mradi wa *ACAI* ili kuainisha mahitaji ya mbolea katika uzalishaji wa zao la muhogo.

## 6.0 Palizi:

Palizi ifanyike mara 2- 3 kwa msimu ili kuzuia magugu ambayo husababisha upotevu wa mavuno. Kurudishia udongo kwenye mashina wakati wa palizi, huongeza mazao



Picha 3: Palizi katika shamba la muhogo

## 7.0 Visumbufu vya muhogo

### 7.1. Magonjwa

**Michirizi ya kahawia** na **Batobato** ni magonjwa makuu yanayoathiri uzalishaji wa zao la muhogo (Picha 4 & 5). Magonjwa haya husababishwa na virusi wanaosambazwa na nzi weupe. Kudhibiti magonjwa haya tumia mbegu bora za muhogo zenye ukinzani pia ng'oa mimea yenye dalili na kuiangamiza.



Picha 4: Ugonjwa wa Michirizi ya kahawia